# *Aga Khan Foundation* na mageuzi ya kuzalisha ufuta

## ■ Mikoa ya Lindi, Mtwara ; wilaya Kilwa zang'ara
## ■ Shamba lililotoa magunia 2, sasa lavuna magunia 8

NA ANGELA SEBASTIAN

**MIKOA ya Kusini mwa Tanzania ikiwemo Lindi la Mtwara, inashamiri katika uzalishaji wa mazao ya kadhaa, ikiwemo ufuta. Lakini maendeleo ya uzalishaji huo bado yanakwama kwa maana ya kwamba hayajapewa kipaumbele.**

Hivi sasa taasisi ya Aga Khan Foundation imejitokeza na kuamua kusaidia maendeleo vijijini katika meneo mwambao wa Pwani ya nchi katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kupitia mpango maalumu uitwao CRSPT au Coastal Rural Support Programme Tanzania.

Lengo kuu hapo ni kufikia hatua hali ya maisha ya wananchi hao inainuka juu na kuzidi kuwaondoa katika umasikini, hata ujinga na maradhi.

Ili kuweka mambo sawa, kunahitaji ubia wa sekta binafsi na ya umma. Huko katika mikoa hiyo ya Kusini mwa Tanzania kumewekwa ubia maalumu katika ya sekta binafsi na ya umma, ambapo Aga Khan Foundation kupitia wataalamu wanaotoa msaada wa mafunzo kwa vitendo na kuwatafutia masoko.

Ni mpango unaohusisha ustawi wa kaya 60,000 katika mikoa hiyo, ikiwa ni njia endelevu ya wao kujiinua.

**MAFANIKIO YA UFUTA**

Rehema Mohamed, ambaye ni mkulima wa zao la ufuta Wilayani Kilwa, anaeleza hali halisi kwa kutumia kauli: "Siku za nyuma nilibweteka sana. Nilikuwa nikiombaomba, lakini leo naweza kujitegemea kwa kila kitu.

"Nina mwanaume, lakini tunasaidiana katika mambo mbalimbali, ikwemo kusomesha watoto wetu wawili. Hayo mafanikio nimeyapata kutokana na kilimo cha ufuta."

Anasema, katika kipindi cha mwaka jana alilima shamba eka tano alizotegemea kuvuna kati ya magunia manane na 10, lakini kutokana na tija katika uzalishaji wake alivuna magunia 11.

Anasema, mafunzo hayo yamemwezesha kutambua mbinu za upandaji bora wa mbegu, kuchanganya mazao katika sehemu moja na maelekezo hayo ya kitaalamu yamemfanya afanikiwe zaidi na matunda mojawapo aliyo nayo ni kwamba, amefanikiwa kujenga bora nyumba ya matofali na kuondokana na nyumba ya miti na udongo aliyotumia zamani na yake.

"Kutokana na mafunzo niliyopata kutoka katika taasisi ya Aga Khan Foundation, yameniwezesha kutambua pembejeo zilizo bora na zinazofaa kwa mahitaji ya wakulima katika maeneo mbalimbali.

"Nimeweza kutafuta mtaji na kuamua kujikita katika biashara ya kuuza viatilifu (mbegu bora na dawa za kuulia magugu na wadudu) ambapo biashara hiyo inalipa kusema ukweli," anasema Kudra Nguiga, ambaye ni wakala wa pembejeo vijijini.

Anataja mafunzo aliyoyapata ni kilimo cha ufuta ambapo kinaendeshwa kupitia utafiti, pia vitendo na sasa ameshakuwa mjuzi katika eneo hilo, ikiwemo kuwatambua walanguzi wa bidhaa zao.

Bibi mwingine mwenye umri wa miaka 78, anayejitambulisha kwa jina la Bimkubwa Amil, anasema yeye analima ufuta na huzalisha kati ya tani moja na mbili za zao hilo kwa msimu. Anafafanua,

"Utaratibu wa kuleta pembejeo kama vile dawa na mbegu bora vijijini imetusaidia sana kuongeza uzalishaji maradufu kwa mazao ya biashara na chakula, kwani wakati Aga Khan walipofika vijijini na kutoa elimu juu ya matumizi bora ya pembejeo kwamba inasaidia kuongeza uzalishaji.

"Tuliona kama vile wanatusumbua, pia ilikuwa ngumu kuzipata katika maeneo yetu kwa urahisi, mpaka wakajitokeza walanguzi na kutuuzia kwa bei ya juu, lakini tulikuwa tukishindwa kununua maana hatukujua matumizi yake na uzuri wake, wakati mwingine waliojitahidi kununua walinunua dawa zilizomaliza muda wake na kujikuta wakiharibikiwa, kwani hatukuwa na utaalamu."


Anasema, kupitia wakala vijijini waliopata mafunzo kutoka Aga Khan, imewezesha wakulima kupata pembejeo hizo kwa urahisi na kuboresha kilimo na kuwaondolea usumbufu wakulima.

"Kupitia wakala hao, tumeweza kumudu bei, pia kuona umuhimu wa matumizi bora ya pembejeo. Kwani, ukilinganisha na wale ambao hawakutumia kwa msimu uliopita na misimu mingine na mimi niliyetumia, kuna tofauti. Mimi nimezalisha zaidi yao," anasema na kuongeza:

"Mtu kalima eka mbili, unakuta anazalisha kati ya gunia na moja na nusu, huku mimi nimelima heka hizo mbili na kuzalisha magunia manne. Kweli hayo si ndiyo mafaniko,"anatamka bibi huyo kwa hamasa ya furaha

**USHAURI WA AGA KHAN FOUNDATION**

Awamu iliyopo ya CRSPT, inatarajiwa kumalizika ▷▷▷ uk. 12-13



MJASIRIAMALI wa kashata za ufuta akiwa kazini.

US

